

## **LATRA yatangaza nauli za treni ya abiria Moshi - Arusha**

Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetangaza nauli za treni ya abiria itakayofanya safari zake kutoka Moshi mjini hadi Arusha na kurudi Moshi. Akizungumza na waandishi wa habari Mkoani Arusha leo tarehe 29 Septemba, 2020, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA Gilliard Ngewe amesema nauli hizo zimetangazwa kufuatia Shirika la Reli Nchini (TRC) kuwasilisha maombi ya nauli hizo, ambapo LATRA ilifanya mikutano ya kupokea maoni ya wadau, kisha kufanya uchambuzi wa maoni hayo pamoja na kuchambua mchanganuo uliowasilishwa na TRC.

Kwa mujibu wa kifungu cha 21 (2) (b) cha Sheria ya LATRA namba 3 ya 2019, baada ya mchakato wa uchambuzi kukamilika, Bodi ya Wakurugenzi ya LATRA imeidhinisha nauli hizo na kuainisha nauli zitakazotumika kwa usafiri wa treni ndani ya mikoa hiyo na nje ya mikoa kama inavyoonekana katika jedwali.

### ***Nauli zilizoidhinishwa na LATRA zikionesha mchanganuo wa vituo vya ndani nan je ya mikoa husika***

	<b>KUTOKA MOSHI KWENDA</b>	<b>Umbali (KM)</b>	<b>NAULI KWA MADARAJA HUSIKA (SHS):</b>	
			<b>Daraja la tatu</b>	<b>Pili kukaa</b>
1	RUNDUGAI	22	1,000	1,500
2	KIKULETWA	31	1,000	1,500
3	KIA	37	1,000	1,500
4	USA RIVER	62	1,500	2,000
5	TENGERU	65	1,500	2,000
6	CHEKERENI	75	1,500	2,000
7	NJIRO	82	1,500	2,000
8	ARUSHA	86	1,500	2,000

	KUTOKA ARUSHA KWENDA	Umbali (KM)	NAULI KWA MADARAJA HUSIKA (SHS):	
			Daraja la tatu	Pili kukaa
1	NJIRO	4	1,000	1,500
2	CHEKERENI	11	1,000	1,500
3	TENGERU	21	1,000	1,500
4	USA RIVER	24	1,000	1,500
5	KIA	49	1,500	2,000
6	KIKULETWA	55	1,500	2,000
7	RUNDUGAI	64	1,500	2,000
8	MOSHI	86	1,500	2,000

***Nauli za wanafunzi kutoka mwanzo hadi mwisho wa safari ni Sh. 300.00 kwa daraja la tatu, na Sh. 400.00 kwa daraja la pili kukaa.***



*Mkurugenzi Mkuu LATRA Gilliard Ngewe akimkabidhi Henry Machoke, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara TRC andiko la nauli zilizoidhinishwa*

Wakati huo huo, LATRA imeiagiza TRC kutekeleza masuala mbali mbali ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya usalama kwa wadau husika, kutumia mfumo wa tiketi za kielektroniki, kutoa ratiba za safari kwa umma, kutekeleza hatua za usalama kudhibiti msongamano wa abiria, kuboresha miundombinu na huduma za kijamii, kuweka kitengo cha huduma kwa wateja na kutangaza nauli zilizoidhinishwa katika vyombo mbalimbali vya habari ili ziwafikie wadau wengi zaidi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara kutoka TRC Henry Machoke aliishukuru Serikali kwa kufufua usafiri wa reli Kanda ya Kaskazini na kuishukuru LATRA kwa kutoa muongozo na bei elekezi.

“Tunaishukuru LATRA kwa kutoa bei elekezi ya usafiri wa treni utakaoanza mwezi ujao kutoka Moshi hadi Arusha” alisema

Alisisitiza kuwa shirika hilo litatoa huduma bora kwa wasafiri ndani ya Mkoa wa Kilimanjaro na Arusha sambamba na huduma za usafiri kutoka Mkoani Dar es Salaam hadi Mkoani Arusha.

**Imetolewa na:**

Kitengo cha Mawasiliano

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini